**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu: +255 26963309/13/14*
*Nukushi: +255 26296 3316*
*Barua pepe: ps@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Mji wa Serikali Mtumba,*
*S. L. P. 2908,*
***40477*-DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

## TANGAZO LA UUZAJI VIWANJA ENEO OLMOT KARIBU NA UWANJA WA MPIRA WA AFCON

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inautangazia umma kuwa inauza viwanja katika eneo la Olmot karibu na kiwanja cha mpira cha AfCON Jijini Arusha.

Bei ya viwanja katika eneo la Olmot ni kama ifuatavyo: - Makazi (TZS. 27,000/= kwa mita za mraba), Biashara (TZS. 32,000/= kwa mita za mraba), Makazi na Biashara (TZS. 29,000/= kwa mita za mraba), Makazi ya Jumla (TZS. 32,000/= kwa mita za mraba), Shule ya Msingi (TZS. 27,000/= kwa mita za mraba), Jengo la Umma (TZS. 25,000/= kwa mita za mraba) na Shule ya Chekechea (TZS. 27,000/= kwa mita za mraba).

Fomu za maombi zitatolewa katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Arusha tarehe 18 Agosti, 2025 kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9.00) alasiri kwa gharama ya kiasi cha TZS. 5,000/= (ambacho hakitarudishwa). **Fomu hizo zitatakiwa kurejeshwa ndani ya siku saba (7) zikiwa zimejazwa kikamilifu pamoja na picha ya mwombaji zikiambatishwa na nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) pamoja na uthibitisho wa malipo ya asilimia ishilini na tano (25%) ya thamani ya kiwanja.**

**Waombaji watatakiwa kukamilisha gharama zote za ununuzi wa kiwanja ndani ya siku 30 tangu tarehe ya maombi. Endapo mwombaji atashindwa kukamilisha malipo hayo, kiwanja husika kitatolewa kwa mtu mwingine bila ilani yoyote kwa mhusika.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya wizara ya *www.lands.go.tz au kituo cha mawasiliano kwa wateja kupitia namba* ***0262161610, 0739646885 na 0736665533****.*

**Imetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
**WIZARA WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**12 Agosti, 2025**